Baadhii ya Watanyakazi wa EWURA wakisisitiza mada kutoka kwa Sajini Mstaafu Alex Ojode (aliyesimama) wa kikosi cha Zimamoto wakati wa mafunzo ya kuzima moto yaliyofanyika katika ofisi za EWURA Juni 2014.



Menjela wa EWURA wa Ufundi wa Maji safi na Usafi wa Mazingira, Mhandisi Exaud Fataeli (mwenye mivwazi) akimkabidhi zawadi maalum B. Katiri Gromenier, wakati wa sherehe ya kumuaga iliyoitanyika ofisi za EWURA, Septemba 2014. Bi Gromenier anarudi Ujerumani, baada ya kumaliza muda wake Tanzania, ambapo alikuwa akifanya kazi EWURA kama Mshauri wa Program ya Maji Tanzania, chini ya msada wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Shirikisho la Ujerumani (GIZ).



Mkurugenzi wa EWURA wa Fedha, Utawala na Rasidimali Watu, Bi Ntunungishu Molei, akipokea zawadi ya ushindi kutoka kwa Naibu Waziri wa Fedha, Bw. Mwigulu Nchemba kwa Mamlaka kuwa mshindi wa kuwasilisha mapema makato ya watumishi wake katika Mkuu wa PPF. Hatia hiyo ilitanyika Septemba 2014 Arusha wakati wa Mkutano wa Mwaka wa PPF.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Kazi Maalum), Profesa Mark Mwandosya (kushoto) akikabidhi kitabu kinachoitwa " Udhidi wa Huduma za Kiuchumi Tanzania", kwa Mwenyekiti wa Bodi wa EWURA, Bw. Simon Sayore, wakati Waziri huyo alipotembelea EWURA, Agosti 2014.



Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Felix Ngamagosi (aliyesimama) akifatanua jambo mbele ya aliyekuwika Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Bashiri Mrindoko, alipotembelea EWURA, mwezi Juni 2014.

Wasilisha malalamiko yako ndani ya muda wa kikomo

Na Michael Mshighwa

Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kupitia Tangazo la Serikali namba 10, imetoa kanuni na taratibu zinazotumiwa na EWURA katika kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za nishati na maji.

Zisizo sahihi na kushindwa ama kukataliwa kuunganishwa kwenye huduma yamwekewa muda kikomo wa miezi kumi na mbili kuwasilishwa EWURA, malalamiko ambayo yanahusisha kuza ama kusambaza bidhaa za petroli zisizo na kiwango yatatakiwa kuwasilishwa EWURA ndani ya siku saba.

Aidha muda kikomo wa kuwasilishwa malalamiko yote yanayohusu uzaji ama usambazaji wa bidhaa za petroli bila kuzingatia bei elekezi ni miezi sita, wakati muda kikomo wa malalamiko yote yanayohusisha huduma mbovu ni miezi ishirini na minne.

Wakati huo huo muda kikomo wa kuwasilishwa malalamiko ambayo hayapo katika makundi yaliyotajwa hapo juu ni miezi kumi na mbili. Sababu hasa ya kutoa muda kikomo wa kuwasilishwa malalamiko ni kuongeza ufansi katika kushughulikia matatizo ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA kwa kuwzesha kupata ushahidi utakaosaidia kufikia uamuzi wa haki.

Hivyo basi ni wajibu wa kila mtumiaji wa huduma za nishati na maji kuzingatia kanuni na taratibu zote zilizowekwa kwenye taratibu za kushughulikia matatizo ya watumiaji ili kuwzesha haki itendek.

Prof.Mwandosya: Anzisheni jumua

Na Wilfred Mwakalosi

Mamlaka za Udhiditi Tanzania zimeaswa kuanzisha jumua itakayozisaidia kuwa na sauti moja yenye nguvu kuwawzesha kusimamia maslahi yao. Mwito huo ulitolewa hivi karibuni na Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais, Kazi Maalum) Prof. Mark Wandosya alipofanya ziara kwenye mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) jijini Dar es Salaam.

Tangu wakati huo, serikali imeanzisha mamlaka nyingine kadhaa kama vile Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Bima (TIRA), Mamlaka ya Usimamizi na Udhiditi wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii (SSRA) na Mamlaka ya Udhiditi wa Mbolea Tanzania (TFRA).

na Menejimenti ya EWURA, kwa mafanikio waliyoyapata

Manufaa ya kuwa na mipango ya kusimamia mali katika mamlaka za maji

Na Titus Safari

Mamlaka za maji huendesha mifumo yenye mali zilizofuikiwa ardhini au zilizoko juu ya ardhini.

Kwa mujibu wa mwongozo wa kusimamia mali za majisafi na majitaka uliochapishwa mwaka 2006 na New Mexico Environmental Finance Centre, mali za mifumo ya majisafi na majitaka zimetafsiriwa kujumuishwa miundombinu kama vile mabomba, matenki, pampu, visima, mitambo ya kutibu maji pamoja na miundombinu mingine inayofanya mifumo mzima wa huduma ya majisafi na majitaka.

Kwa kadiri muda unavyokwenda mali hizi hupungua thamani au uwezo wake wa kutoa huduma kutokana na umri na uchakavu. Matokeo yake ni kwamba inakuwa vigumu kwa mamlaka husika kutoa huduma za kuridhisha kwa wateja wake na pia gharama za uendesaji na matengenezo huwa kubwa kuliko kawaida. Gharama za uendesaji na matengenezo zinapokuwa kubwa huguka pia kuwa mzigo kwa wateja ambao watalazimika kupipa bei kubwa zaidi ili waweze kuendelea kupata huduma.

Dhana ya Usimamizi wa Mali inatoa mwongozo wa jinsi ya kufanya maamuzi kuhusu mali hizo kwa namna itakayowezesha utoaji wa huduma endelevu ya maji.

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Kimataifa wa Usimamizi wa Miundombinu (International Infrastructure Management Manual) wa mwaka 2002, Usimamizi wa Mali umetafsiriwa kuwa ni muunganiko wa taaluma za utawala, fedha, uchumi, uhandisi pamoja na taaluma nyingine kwenye mali ili kuziwezesha kutoa huduma inayotakiwa na kwa gharama nafuu zaidi.

Inaendelea kufafanuliwa kuwa lengo la kusimamia mali ni kutoa huduma kwa kiwango kinachotakiwa na kwa gharama nafuu zaidi kwa kuzingatia maamuzi bora kuhusu mali katika hatua za ujenzi, ununuzi, uendesaji, matengenezo, ukarabati na uondaji wa miundombinu iliyochoakaa kwa faida ya wateja wa sasa na wa baadaye.

Kwa maneno mengine, huu ni utaratibu wa kusimamia mali kwa namna ambayo itapunguza gharama ya ununuzi

pamoja na uendesaji na matengenezo na wakati huo kukidhi kiwango cha huduma kinachohitajika na wateja pamoja na wadhhibiti katika huduma zinazotolewa.

Mipango wa kusimamia mali unajumisha uchambuzi wa kazi zitakazofanywa, rasiliimaji zitakazotumika, wahusika na muda wa kutekeleza mkakati wa kusimamia mali hizo.

Mwongozo wa kusimamia mali uliochapishwa na taasisi ya Marekani iliitwayo United States Environmental Protection Agency (EPA) mnamo mwaka 2008 unafatana maswali matano ambayo mamlaka ya maji inapaswa kuyajibu katika kuandaa mpango wa kusimamia mali.

Utafiti uliofanywa na taasisi ya McGraw-Hill Construction na kuchapishwa kwenye ripoti yake ya mwaka 2013 iliitwayo Smart Market Report umeainisha, pamoja mengine, faida ya kuwa na Mipango ya Kusimamia Mali kwa makampuni yanayotoa huduma za maji.

Pamoja na mambo mengine, ripoti hiyo inataja faida kuu tatu za kwanza ambazo ni kuongeza uwezo kuelezea, kuchambua na kujenga hoja za kutea bajeti za uwekezaji, kutambua vipaumbele vya mamlaka na kuwa na utahamu mpana wa matokeo ya maamuzi ya uwekezaji katika miundombinu yao.

Mamlaka za maji zenye mipango thabiti ya kusimamia mali zao hutoa mapendelezo ya uwekezaji kwa kuzingatia tathmini ya hali halisi ya maji zao, athari na matokeo katika utoaji wa huduma pamoja na maswala ya kimazingira na kijamii.

Mtazamo huu huziwezesha mamlaka za maji kufanya maamuzi bora zaidi na pia kupipa takwimu zinazoweza kuwasilishwa kwa watoa fedha pamoja na taasisi za udhibiti. Kwa ufupi, mtazamo huu huwezesha mamlaka za maji kupanga miradi ya uwekezaji kwa kuzingatia hoja za msingi.

EWURA yaidhinisha mabadiliko ya bei kwa mamlaka 19 za maji

Na Titus Safari

Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeidhinisha marekebisho ya bei za huduma za maji kwa mamlaka 19 za majisafi na usafi wa mazingira.

Marekebisho hayo ya bei za maji yamefanyika ili kuziwezesha mamlaka hizo kumudu kuipia ankara za umeme ambazo zimeongezeka kutokana na kuongezeka kwa bei ya umeme kwa asilimia 39.19 kuanzia tarehe 1 Januari, 2014.

Mamlaka hizo 19 ni Arusha, Babati, Bariadi, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, KASHWASA na Kigoma. Mamlaka nyingine katika orodha hiyo ni Lindi, Mbeya, Morogoro, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Singida, Songea, Tabora na Tanga. Maombi ya marekebisho ya bei kutokana na kupanda kwa bei ya umeme yaliwasilishwa kati ya tarehe 8 Januari 2014 na 13 Februari 2014.

Baada ya kupokea maombi hayo na kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) cha Sheria ya Mamlaka ya Huduma za Nishati na Maji, Cap 414, EWURA ilitanya taffishi ili kuona uhalali wa bei zilizopendekezwa.

Taffishi hii ilijumuisha tathmini ya kiuchumi na kifundi ya maombi yaliyowasilishwa na kukusanya maoni ya wadau kati ya tarehe 28 Februari na 13 Machi 2014.

Wakati wa kukusanya maoni ya wadau, Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) na Baraza la Watumiaji wa Huduma Zinzodhibitiwa na EWURA (EWURACC) walichambua na kutoa maoni yao kuhusu uhalali wa maombi ya kurekebisha bei za maji kutokana na kupanda kwa bei ya umeme.

Maoni ya GCC na EWURA CCC yalizingatiwa wakati wa kufanya tathmini. Pamoja na hayo, wananchi wote walipewa fursa ya kuwasilisha kwa EWURA maoni yao

Miundombinu ya kusafisha maji, Mamlaka ya Maji Tanga.



kwa maandishi kuhusu maombi hayo. Hata hivyo, hakuna maoni yaliyopokelewa kutoka kwa wananchi. Kutokana na taffishi na tathmini iliyofanyika, EWURA ilihitimisha kuwa ilikuwa ni halali kuongeza bei za maji isipokuwa si kwa kiwango kikubwa kilichopendekezwa na mamlaka za maji.

Mamlaka za maji zilipendekeza bei zao mpya kwa kuzingatia wastani wa ongezeko la bei za umeme kwa asilimia 39.19, badala ya ongezeko halisi la bei za umeme kwa mamlaka hizo ambalo linategemea ongezeko halisi katika kundi la bei ya umeme ambayo mamlaka inalipa. Kwa kuzingatia ongezeko halisi kwa makundi ya bei za umeme, makundi mengine yalipata ongezeko la chini ya asilimia 39.19. EWURA ilirekebisha bei za maji kwa kuzingatia ongezeko halisi la bei za umeme kwa mamlaka za maji.

EWURA ilitoa Agizo la Marekebisho ya Bei kwa kila mamlaka iliyowasilisha maombi. Hata hivyo, bei hizo zilizo dhidi zinaambatana na masharti yaliyomo katika maagizo yaliyotanguka. Bei hizo zilizo dhidi hini zilianza kutumika tarehe 1 Aprili 2014.

EWURA wapewa mafunzo ya kuzima moto

Na Wilfred Mwakalosi
Watumishi wa Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hivi karibuni walishiriki mafunzo ya kuzima moto. Mafunzo ambayo yaliendeshwa na wakufunzi kutoka Kikosi cha Zimamoto Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na EWURA kwa lengo la kuwapa ujuzi watumishi wake kuhusu hatari za moto, vyanzo vyake, uziaji na namna ya kuzima moto kwa kutumia vitaa stahiki. Mkufunzi Mkuu wa Kikosi cha Zima Moto Staff Sajenti Alex Ojode alisema ingawa moto umekuwa ratiki wa binadamu kwa miaka mingi, bado ndiyo chanzo kikubwa cha uharibifu wa maisha na mali ulimwengu kote.

Mafunzo hayo ya siku moja yalianza kwa mhadhara na kazi za darasani, na kumalizia kwa mafunzo kwa vitendo, kwa kuzima moto halisi kwenye ufukwe, karibu na hospitali ya Aga Khan. Baadhi ya watumishi walioshiriki walisema mafunzo hayo ni muhimu, na kwamba yatawasaidia si wao tu, bali pia wanatamili na jamii kwa ujumla kwenye maeneo yao ya makazi.

Baadhi ya wafanyakazi wa EWURA wakishiriki mafunzo ya kuzima moto: Bt.Christine Mipama (kushoto) na Bw. Francis Mhina wakionyesha namna ya kutumia blanketi maalum ya kuzima moto.



Manufaa ya udhibiti wa EWURA kwenye uchumi sasa yadhahirika

- Mwaka 2008 bei ya petroli kwa Dar ilifika TZS 2,200
- Januari 2009 EWURA ilishusha hadi kufika TZS 1,147
- Oktoba 2014, petroli TZS 2,192 bado haijavuka ya miaka 6
- Bei ingekuwa kiasi gani sasa kama EWURA isingekuwapo?

Na Titus Kaguo

UTAFITI wa hivi karibuni uliofanaywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kutathmini manufaa ya udhibiti wa EWURA kwenye biashara ya sekta ya petroli nchini Tanzania, umeonesha kuwa watumiaji wamefaidika kwa kuokoa shilingi bilioni 124.7 kutokana na kuwepo kwa bei kikomo. Utafiti umethibitisha kuwa kuanzishwa kwa uwekaji wa bei katika bidhaa za mafuta ya petroli kumeshusha bei kwa wastani wa shilingi 110 petroli, shilingi 96 dizeli na shilingi 123 kwa mafuta ya taa, kuanzi a Julai 2009 hadi Juni 2010.

Mpango huo ulisaidia watumiaji kuokoa shilingi bilioni 124.7 na hivyo kufanya kuwepo ongezeko la matumizi mengine na kuchangia kwenye uchumi wa nchi kwa shilingi bilioni 445.5 ambazo ilifanya Serikali kuongeza kukusanya kodi kwa shilingi bilioni 49 (asilimia 1.1 ya ukusanyaji wa kodi kwa mwaka 2009/2010 kwa kuongeza matumizi yenye stakabadhi).

Utafiti huo unafanua zaidi kuwa kuwepo kwa bei isiyoyumba katika bidhaa za petroli, kulisaidia kuwepo mipango mizuri ambayo iliwapa manufaa ya watu masikini. Uthabiti wa bei uliongeza pia uwezo wa ukusanyaji kodi kutokana na kuwepo kwa vipato vionavyotabirika.

Kwa mujibu wa utafiti huo ulioongozwa na Profesa Haji Semboja, EWURA imepongezwa kwa kupata mafanikio makubwa tangu kuanzishwa kwaka mwaka 2006.

"Hata hivyo, moja ya changamoto ambazo EWURA inapata ni kuonesha kwa takwimu kwa baadhi ya mafanikio haya kwa kuboresha mikakati ya udhibiti kwa baadhi ya sekta," inasema sehemu ya taarifa hiyo na kuongeza: " Biashara katika sekta ndogo ya petroli ni eneo mojawapo ambalo imeonesha mafanikio kwa takwimu kutokana na udhibiti

ambao umefanyika kwa sababu ya umuhimu kwa kodi ya Serikali." Takwimu kwa manufaa yanayoonekana katika udhibiti unahitajika ili kuangalia kwa namna gani udhibiti umesaidia kuboresha ukusanyaji wa kodi na hivyo kuboresha maisha ya Watanzania. Pia utafiti uliangalia kama kodi kutoka katika bidhaa za petroli uliongezeka kwa uwingi na uwiano wa kodi zote, hasa ikizingatiwa kuwa udhibiti wa EWURA katika bidhaa za petroli upo pia katika uzaji wa mafuta ya nje ndani ya nchi, uchakachaji na uingizaji kwa mafuta kwa pamoja. Utafiti ulitumia njia nyingi katika kufanikisha taarifa yake pamoja na mambo mengine; kuangalia kazi za ofisini, historia ya biashara ya bidhaa za petroli na kufanya utafiti kwenye maeneo ya biashara ya maeneo kwa maeneo yaliyochaguliwa ya mikoja na taasisi. Utafiti ulifanya tathmini ya manufaa ya udhibiti katika maeneo manne; kuweka vinasaba ili kuzuia uchakachaji na uzaji wa mafuta ya nje ndani ya nchi, kuanzishwa kwa uingizaji wa mafuta kwa pamoja na uanzishaji wa bei kikomo.



Bei kikomo kwa bidhaa za mafuta ya petroli imesaidia kuokoa shilingi bilioni 124.7 hadi kufika Juni 2010.

EWURA yaendeshwa mafunzo ya matumizi ya mafuta yenye salfa kidogo

Na Titus Kaguo

Mamlaka ya Udhidhiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeongeza nguvu katika utoaji wa elimu kwa wadau wa biashara ya sekta ndogo ya petroli nchini kote. Tayari Mamlaka imeshaeendeshwa mafunzo hayo kwa wadau wa masuala ya Petroli kwa mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kagera na Shinyanga.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Petroli wa EWURA, Mhandisi Godwin Samwel, mafunzo hayo yameleaga, pamoja na mambo mengine, kuwahamasisha wadau wa mafuta ya petroli jinsi ya kufanya biashara ya mafuta kwa kutekeleza miongozo iliyowekwa katika biashara hiyo.

Mhandisi Samwel pia anasema mafunzo hiyo yameleaga kuwatundisha wadau juu ya umuhimu wa matumizi ya mafuta yenye kiwango kidogo cha salfa, kuwatataifu wadau madhara ya kutumia mafuta yenye salfa nyingi; kuwapa taarifa hatua ambazo Serikali imezichukua; na mipango iliyopo ya kupunguza kiwango cha mafuta yenye salfa nyingi nchini Tanzania; na kubadilishana mawazo kuhusu mwenendo wa matumizi ya mafuta yenye kiwango kidogo cha salfa kwa Tanzania, barani Afrika na maeneo mengine duniani.

Kwa Dar es Salaam, mafunzo yalitanyika tarehe 20 Aprili, 2014 ambapo wadau 63 walihudhuria. Wadau waliipongeza EWURA kwa kutoa mafunzo hayo ambayo waliyaona yanaelimisha sana juu ya masuala ya usalama na utunzaji wa mazingira.

Mafunzo hayo yamekuwa yanajikita zaidi kwenye kuangalia hali ilivyo ulimwenguni, madhara ya kutumia mafuta yenye salfa nyingi dhidi ya ndogo, utekelezaji wa sheria juu ya matumizi ya salfa kidogo nchini Tanzania, gharama ya kutekeleza agizo la kutumia mafuta yenye salfa kidogo nchini Tanzania na nini kifanyike hapo baadaye.

Washiriki wa semina ya kuhamasisha matumizi ya mafuta yenye kiwango kidogo cha madini ya salfa, iliyofanyika Gold Crest Hotel, Mwanza, Agosti 12, 2014. Waliokaa kutoka kulia ni Mhandisi Godwin Samwel, Mkurugenzi wa Petroli EWURA, Mhandisi Evarist Ndikilo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Gerald Maganga, Meneja wa Ufundi wa petroli EWURA, na Bi. Christina Owenya, Afisa Biashara wa Mkoa wa Mwanza.



Mafunzo ya mwisho kwa awamu hii yalitanyika Mjini Kahama tarehe 18 Agosti 2014, ambapo wadau 19 walihudhuria. Mamlaka kwa sasa inajipanga kuendeshwa warsha za mafunzo hayo kwa mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Ruvuma, Rukwa na Katavi, Nyanda za Juu Kusini na malengo ya Mamlaka ni kutoa elimu hiyo kwa mikoa yote itikapo Juni 2015.

Mkurugenzi Mkuu mpya EWURA ataja vipaumbele yake

Titus Kaguo na Wilfred Mwakalos!

Baada ya kukalia kiti kipya, Mkurugenzi Mkuu mpya wa Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Bw. Felix Ngamliagos! ametaja vipaumbele sita anavyovifanyia kazi.

Bw. Ngamliagos!, aliyechukua nafasi ya aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu tangu Februari 1, 2014 anataja kipaumbele cha kwanza kuwa ni kuanzisha ofisi za Mamlaka katika kanda zote hapa nchini ili kupeleka huduma kwa wadau. Mamlaka inatarajia kufungua ofisi za kanda katika maeneo manne ya Ziwa, Kaskazini, Kati na Nyanda za Juu Kusini. Ameihakikishia serikali, umma na wadau wa Mamlaka kuwa kwa EWURA kufuata sheria na kanuni za udhibiti wa kimataifa ni kipaumbele cha pili, kwa mujibu wa Bw. Ngamliagos!.

Majukumu mengine ya Mkurugenzi Mkuu mpya yatakuwa ni kushamirisha uwekezaji katika sekta ya nishati jadidifu hususani katika kuongeza upatikanaji wa umeme na kuwepo kwa matumizi ya vyanzo mbadala vya umeme.

“Kuhakikisha kunakuwepo na kushindani wa haki kwa watoa huduma wa jumla na wauzaji wa rejareja katika bidhaa za mafuta ya petroli, kitakuwa ni moja ya vipaumbele vyanгу, ili Watanzania wafaidike na upatikanaji wa mafuta,” alisema Bw. Ngamliagos!.

Kipaumbele cha mwisho kwa mujibu wa Bw. Ngamliagos!, kitakuwa ni kwa EWURA kushiriki kikamilifu katika kuendeleza Sera ya Gesi Asili na kutekeleza sheria ili kuhakikisha sekta hiyo inaleta maendeleo endelevu kwa faida ya Watanzania wote.

Bw. Ngamliagos! alijaza nafasi iliyoachwa wazi na Bw. Masebu, ambaye muda wake wa miaka minane kwa mujibu wa Sheria ya EWURA Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania uliisha Desemba 31, 2013.

Ni mtaalam katika masuala ya udhibiti wa mashirika na kampuni za nishati na maji, akibobea hasa kwenye eneo la kutathmini bei za huduma hizo, kuinda wataji na ubunifu wa njia mwafaka za mawasiliano na wadau wa sekta za umeme, petroli gesi asilia na maji.

Kabla ya kuteuliwa, Bw. Ngamliagos! alikuwa Mkurugenzi Mdhibiti Uchumi, nafasi ambayo amefanya kazi kwa miaka saba. Uteuzi wa Bw. Ngamliagos! umepongezwa na wengi, hasa kwa kuwa anafahamika kwa namna ambavyo anapenda kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia viwango vya kiudhibiti na ushirikishwaji wa wafanyakazi.

Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA Bw. Simon Sayore amesema: “Kwa uzoefu wake mkubwa kwenye tasnia zinazodhibitiwa na EWURA, Bw. Ngamliagos! anategemewa kutekeleza majukumu na kazi zake kwa uaminifu na weledi wa hali ya juu.”

Bw. Ngamliagos! ana shahada ya Uzamili katika masuala ya uchumi kutoka Chuo cha Fedha Moscow, Urusi (1990 – 1996); astashahada ya masuala ya Sera na Mipango ya Miradi kutoka Taasisi ya Masuala ya Sayansi ya Jamii, (ISS) The Hague – Uholanzi, (mwaka 2000) na Cheti cha Full Technician Certificate katika uhandisi wa Maji kutoka Chuo Cha Maji (1984 – 1987).

Pia ni mtaalam anayetambulika wa masuala ya Udhiditi, ambapo alitunukiwa cheti kwa pamoja kati ya Taasisi ya Public-Private Partnerships (IP3) ya Washington, Marekani; na Kituo cha Maendeleo ya Uhandisi wa Maji cha chuo kikuu cha Loughborough (WEDC/LU) cha Uingereza (2013).

Ni mtaalam katika masuala ya udhibiti wa mashirika na kampuni za nishati na maji, akibobea hasa kwenye eneo la kutathmini bei za huduma hizo, kuinda wataji na ubunifu wa njia mwafaka za mawasiliano na wadau wa sekta za umeme, petroli gesi asilia na maji. Kabla ya kujiunga na EWURA, Bw. Ngamliagos! alifanya kazi Wizara ya Maji, Nishati na Madiini, na baadaye Wizara ya Maji, kwa jumla ya miaka 17 kwenye ngazi mbali mbali, na kupanda vyeo hadi kufikia Mchumi Mwandamizi.

Kutaka Dawati la Mkuugenzi Mkuu

Mpenzi msomaji,

Ninakukaribisha kwa furaha kusoma toleo hili la mwezi Septemba la jarida la Mamlaka ya Uchibiti wa Huduma za Nishati na Maji, iliulikanalo kama jarida la EWURA, nikiwa Mkurugenzi Mkuu mpya na pia Mwenyekiti wa Jarida hili.

Ninawashukuru kwa dhati kwa kutuunga mkono bila kuchoka, kwani bila ninyi ingekuwa vigumu mno kwa mamlaka kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Ninawashukuru pia kwa namna mlivyompa ushirikiano Mkurugenzi aliyenitanguilia, Bw. Haruna Masebu, katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa ajili ya nchi hii.

Wakati natambua na kuheshimu jitihada zote zilizofanywa na uongozi uliopita, ambao kwa kwele uliitahidi bila kuchoka kuweka msingi imara na thabiti, ambao EWURA inaufurahia leo, nina mtazamo wa kuendelea kufanya kazi juu ya msingi huo imara ili kuhakikisha kwamba EWURA inaendelea kuhudumia wadau wake kwa weledi wa hali ya juu. Ninapenda kuhakikisha serikali, wadau na umma kwa ujumla kuwa Mamlaka inaahidi kuendelea kutimiza wajibu wake kwa kufuata mbinu bora za kimataifa na kuheshimu utawala wa sheria.

Ili kufikia lengo hilo, kipaumbele chetu cha kwanza ni kuanzisha ofisi za kikanda nchi nzima, tukiwa na lengo la kufikisha huduma zetu kwa watoa huduma na watumiaji wa huduma hizo pia. Mamlaka inatarajia kufungua ofisi kwenye kanda mne za Ziwa, Kaskazini, Kati na Nyanda za Juu Kusini.

Jambo lingine kubwa kwenye kipindi hiki ni uzinduzi wa ripoti ya utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, iliyobaini manufaa makubwa yaliyopatikana kwa EWURA kudhibiti ipasavyo sekta za uchumi, hususan sekta ndogo ya petroli, ambapo mabilioni ya shilingi yameokolewa na kubakia mifukoni mwa watumiaji huduma zinazodhibitiwa.

Ni dhahiri kwamba umuhimu wa EWURA kama mdhibiti upo, utaendelea kuwepo, na ningeomba wadau kutupa ushirikiano wa hali ya juu ili tuendelee kufanikisha azma yetu ya kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

EWURA pia itaongeza jitihada zake katika kuweka mazingira rafiki kwa uwekezaji, hususan kwenye sekta ndogo ya nishati ya umeme, ili kuongeza idadi ya watumiaji umeme na kuhamasisha matumizi ya vyanzo mbadala vya uzalishaji umeme, hasa hasa sekta ndogo ya Nishati Jadidifu nchini. Mamlaka itaendelea pia kuwa mshiriki thabiti katika utayarishaji wa Sera ya Taifa ya Gesi Asilia na sheria zake, ili kuhakikisha kuwa sekta hiyo inadhitiwa ipasavyo kwa faida ya Watanzania wote. Ni kwa faida ya wadau wetu wote pia kwamba uwepo wa ushindani na fursa sawa za uwekezaji kati ya wafanyabashara wa jumla na wale wa rejareja wa bidhaa za petroli unapewa mtazamo maalum ili kuwanufaisha Watanzania.


Kwa heshima kubwa ninawaomba wapenzi wasomaji na wadau kwa ujumla kuendelea kushirikiana na EWURA, kama ambavyo mmekuwa mkitanya huko nyuma, kwa faida ya ustawi wa kiuchumi na kijamii wa Taifa letu.

Karibuni!

Bw. Felix Ngamlagosi



Wataka wa Mhavi



Bw. Titus Kaguo

KARIBU katika toleo la Jarida la 11 la Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Toleo hili, linakuja wakati kumekuwa na mabadiliko ya uongozi wa juu katika Mamlaka, ambapo Bw. Felix Ngamliagosi—mmoja wa wajumbe ya Bodi ya Uhariri ya Jarida hili na ambaye alikuwa Mkurugenzi Mdhiditi Uchumi, amekuwa Mkurugenzi Mkuu, tangu Februari 2014.

Bw. Ngamliagosi anajaza nafasi iliyoachwa na Bw. Haruna Masebu, ambaye kipindi chache cha uongozi kilishiha tarehe 31 December, 2013, baada ya kuiongoza Mamlaka kwa vipindi viwili vya miaka mine-mine, kwa mujibu wa Sheria ya EWURA, sura Namba 414 za Sheria za Tanzania.

Kutokana na hayo, nina furaha kuwataarifu wapendwa wasomaji wetu kuwa Bw. Ngamliagosi amekuwa pia ndiye Mwenyekiti mpya wa Bodi ya Tahariri, hivyo basi, atawajibika kusimamia uendeshaji wa Jarida.

Jarida la EWURA, limeongezeka kuwa ni moja ya nyezo bora za Mamlaka za kutoa taarifa kwa umma, na kwa kufanya hivyo, elimu kwa umma juu ya kufahamu wa masuala ya udhibiti, inaimarishwa.

Hali hii inathibitishwa na kuongezeka kwa idadi ya malalamiko yanayopokelewa na Mamlaka kutoka kwa watumaji, ambao hawaridhishwi na huduma zitolewazo na watoa huduma. Malalamiko mengi yanayowasilishwa yamesikilizwa na kutolea uamuzi.

Katika toleo hili, kuna taarifa nyingi za kufurahisha zinazohusiana na masuala ya mtumo bora wa udhibiti, na hivyo itaendeleza uelewa zaidi kwa umma juu ya masuala ya udhibiti.

Mpendwa msomaji ungana nasi usome habari hizi za kufurahisha.

3	Waraka wa Mhariri.....
4	Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu.....
6	Ewura yaendeshwa mafunzo ya matumizi ya mafuta yenye salfa kidogo.....
7	Manufaa ya udhibiti wa EWURA kwenye uchumi sasa yadhahirika.....
8	EWURA wapewa mafunzo ya kuzima moto.....
9	EWURA yaidhinisha mabadiliko ya bei kwa mamlaka 19 za maji.....
10	Manufaa ya kuwa na mipango ya kusimamia mali katika mamlaka za maji.....
11	Wasilisha malalamiko yako ndani ya muda wa kikomo.....
11	Prof.Mwandosya: Anzisheni jumla.....
12	Habari katika picha.....

Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais, kazi maalum) Prof. Mark Mwandosya, (waliokaa, katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Wakurugenzi wa Bodi ya EWURA na Menejimenti. Kushoto ni mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Bw. Simon Sayore, na kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa EWURA Bw. Felix Ngamlagosi.



Jarida lililopita:

BODI YA UHARIRI

MWENYEKITI

Bw. Felix Ngamlagosi

MHARIRI

Bw. Titus Kaguo

MHARIRI MSAIDIZI

Bw. Wilfred Mwakalosi

WAJUMBE

Bi. Miriam G. Mahanyu

Inf. Charles S. Omjuni

SEKRETARIAT

Ms. Hava Lweno

Ms. Janet Mwaipopo

OFISI ZA EWURA

Ghrofa ya 6,

Jengo la Harbour View Towers

Barabara ya Samora

S.L.P. 72175,

Dar es Salaam, Tanzania.

Simu: +255 (22) 2123850 / 3 / 4 / 6

Faksi: +255 (22) 2123180

Barua pepe: info@ewura.go.tz

www.ewura.go.tz



Manufaa ya udhibiti wa EWURA kwenye uchumi sasa yadhihirika

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 011

OKTOBA 2014

Newsletter

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority

HALIUZWI